

# MAIR

Ripoti ya Mwaka ya Utekelezaji  
MKUKUTA - 2006/2007



**Mipango na Bajeti**

MKUKUTA unatekelezwa na kugharamiwa na serikali pamoja na wadau wengine nje ya serikali. Hii inamaanisha kwamba MKUKUTA unapaswa kuonekana kwenye bajeti za wadau ili kuhakikisha kuwa utoaji wa fedha unatabirika na kufanyika kwa wakati.

Mfumo wa bajeti ya Mkakati wa awali wa Upunguzaji Umaskini ulitenga bajeti kwa sekta chache tu za kipaumbele. MKUKUTA unatambua kwamba sekta zote zinachangia katika juhudi za kukuza uchumi na kupunguza umaskini. Hii imepelekea kuwa na mwelekeo wa kutegemea matokeo ambao unahusisha wadau wengi.

## **MKUKUTA na Bajeti ya Taifa**

Bajeti iliyopitishwa kutekeleza MKUKUTA mwaka 2006/07 ilikuwa ni asilimia 48 ya bajeti yote. Asilimia 52 iliyobakia ilikuwa kwa ajili ya miradi na programu zisizo na uhusiano wa moja kwa moja na MKUKUTA. Mgawanyo wa bajeti iliyotengwa kwa ajili ya MKUKUTA ulikuwa 46% kwa nguzo kwanza, 36% nguzo ya pili, na asilimia 18 kwa nguzo ya tatu. Mgawanyo huu unashabihiana na lengo la kukuza uchumi na kuongeza kipato cha watu maskini zaidi.

Kwa kipindi cha muda wa kati, msisitizo utabaki katika kuweka vipaumbele na kufuatanisha shughuli za MKUKUTA zenye matokeo mengi. Ili kudumisha vigezo vya kiuchumi, bajeti itatenga rasimali zaidi kwa ajili ya matumizi yenye kukuza uchumi wenye kujali watu maskini zaidi. Kwa hiyo tunaweza kutegemea bajeti kubwa zaidi kwa ajili ya maendeleo ya miundombinu kwa uwiano wa ongezeko kwenye huduma za jamii. Tunaweza pia kutarajia mikakati yenye kulenga kupunguza tofauti baina ya mikoa na yenye kujumuisha masuala mtambuka.

## **Kuboresha Michakato ya Bajeti na Ugharamiaji**

Ni muhimu kutenga na kutoa fedha kwa wakati. Hii inamaanisha uboreshaji wa michakato ya bajeti na utoaji wa mafungu ya fedha.

Bado ziko changamoto kuhusiana na namna fedha zinavyotolewa kila mwaka. Utaratibu unatofautiana kati ya Wizara moja na nyingine kutegemeana na mahitaji, na upatikanaji wa raslimali. Matatizo mawili makubwa ni udhaifu wa mipango ya utuaji wa fedha na udhaifu katika uingizaji wa raslimali kwenye Hazina.

Sehemu kubwa ya Bajeti ya Maendeleo inagharamiwa na Wabia wa Maendeleo. Makisio hupitishwa mapema, hata hivyo changamoto inakuwa katika kukabiliana na tatizo la ucheleweshaji na kutotabirika kwa utoaji wa fedha.

Pia kuna tatizo katika kukadiria uhusiano baina ya matumizi ya fedha na matokeo yake kwenye jamii. Hili linaazidi kuwa gumu pale inapochukua zaidi ya mwaka kuweza kwa matokeo kuanza kuonekana. Hili ni tatizo kwa viashira vingi vya MKUKUTA na halina budi kuzingatiwa.

## **Njia za Kuripoti Bajeti**

Bajeti ya taifa huwa katika viwango vya mfumo wa kimataifa wa Takwimu za Fedha za Serikali wakati MKUKUTA hutumia mfumo wa Bajeti wa Upangaji Fedha Kimkakati (SBAS) katika kubainisha namna unavyotumia raslimali. Hii inamaanisha kwamba takwimu za bajaeti za MKUKUTA zinapaswa kubadilishwa ili kuendana na mfumo wa kimataifa wa Takwimu za Fedha za Serikali. Ili kurahisisha mambo, serikali inaandaa muundo wa MKUKUTA wa uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa bajeti. Hii itatoa taarifa kupitia Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti.

Hivi sasa uhusiano wa sera na utekelezaji wa bajeti hupimwa kwa

- Kulinganisha migawo ya SBAS na matumizi halisi
- Kwa kuangalia matokeo yake kwenye umaskini kwa kutumia Mfumo wa Ufuatiliaji wa MKUKUTA.

Mapitio ya Bajeti huhusisha fedha taslimu za serikali, lakini

- Hayahusishi miradi inayogharamiwa moja kwa moja na Wabia wa Maendeleo, na
- Huchukulia upelekaji wa fedha kwenye Serikali za Mitaa kama matumizi.

Mfumo wa sasa unashindwa kushughulikia ugumu uliopo katika ngazi ya wilaya kutokana na kuwepo vyanzo mbali mbali vya ugharamiaji wa programu katika ngazi hiyo. Ugumu huu kwenye mchakato wa bajeti unahitaji marekebisho katika mtiririko wa fedha na kuhakikisha kuwa mfumo unabaki kuwa wa uwazi.

Kwa hiyo, katika mwaka unaofuata wa utekelezaji wa MKUKUTA, mifumo ya uainishaji na utoaji taarifa itaanzishwa ili kurahisisha ukusanyaji na utoaji ripoti ya taarifa toshelevu za fedha. Ili kufanikisha mchakato huu, wadau mbali mbali hususan wabia wa maendeleo na taasisi zinazonufaika zitapaswa kuanza kutumia mifumo jumuishi ya ugharamiaji na utoaji wa taarifa.

Serikali ya Tanzania ilianza kutumia Mkakati wa Pamoja wa Misaada (JAST) Desemba 2006. JAST ni matokeo ya mashauriano yenye wigo mpana yaliyoongozwa na serikali kati ya wabia wa maendeleo na wadau wasiokuwa wa kiserikali. Mkakati huu una akisi nafasi ya serikali katika kuoanisha msaada wa wahisani. Malengo makuu ya JAST ni (a) kupunguza zaidi gharama za uhamishaji fedha (b) kukuza umiliki wa kitaifa na uongozi wa serikali wa ajenda ya maendeleo.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na:**

Wizara ya Fedha na Uchumi,

S..L.P. 9111, Dar Es Salaam

Simu: +255 2111174, Fax: 21103226

Barua Pepe: [mkukuta@gmail.com](mailto:mkukuta@gmail.com); Tovuti: [www.povertymonitoring.go.tz](http://www.povertymonitoring.go.tz)